
# AFRI TWENDE

Kulitia moyo kanisa kwa ajili ya kazi ya kueneza injili ulimwenguni



Jarida la 1, Toleo la 3

WWW.AFRIGO.ORG/AFRI-TWENDE

## Furaha ya Mchungaji: Kanisa Linalojali Umisheni

# YALIYOMO











## 03 MAONI YA MHARIRI

## 04 WACHUNGAJI NA MAONO YA UMISHENI

Ushauri ufaao wa kukusaidia wewe kulitambulisha kanisa lako kwenye ulimwengu wa kimisheni. Jinsi ya kutia moyo wale waliojitoa kwa moyo wao wote katika kujihusisha na umisheni.

## 05 MOYO MKUU WA UMISHENI

Tunaondoka kwenye mazingira yetu ya karibu ili kuwashirikisha wengine habari za Injili. Kwa sasa hili ndilo jambo la kufurahia!

## 06 WAJIBU WA MCHUNGAJI KATIKA KUANZISHA KANISA LENYE MTAZAMO WA UMISHENI

Kuwafikia wengine kwa injili kuna gharama - itakugharimu muda, fedha na hata maisha yako.

## 07 NENDA! HABARI ZA KANISA LA AFRIKA LINALOHAMASISHA UMISHENI

## 08 MAKUNDI YA WATU: WADATOOGA


© 2022 **AFRITWENDE**

**AFRITWENDE** ni chapisho linalotolewa kwa kila robo ya mwaka likiwa na kusudi la kuinua kiwango cha uelewa, kuhamasisha, kufundisha na kutia moyo makanisa na mtu mmoja mmoja binafsi katika Afrika kuhusu umisheni wa kiulimwengu.

**Ubunifu:** Pilgrim Communications


**Picha ya jalada:** Warwick Walker

Picha za mnato zimetumika katika matukio machache. Kwa sababu ya kiusalama yametumika majina ambayo si halisi.

Maoni yaliyomo katika makala mbalimbali ya jarida hili siyo lazima yawe ni ya mchapishaji tu.

# KUTAFAKARI TENA SOMO LA ANTIOKIA

## JE, WACHUNGAJI WANASIKILIZA?



Sura ya 13 ya kitabu cha Matendo ya Mitume inaelezea kanisa ambalo lilikuwa katika sehemu ya Shamu (kwa sasa ni nchi ya Syria) ambalo lilikuwa ni la kwanza kutuma rasmi wamishenari kwenda nchi nyingine, kwenye utamaduni mwingine katika kipindi cha kanisa la Agano Jipya.

*"Na katika kanisa la huko Antiokia, palikuwa na manabii na walimu, nao ni Barnaba, na Simeoni aitwaye Nigeri, na Lukio Mkirene, na Manaeni aliyekuwa ndugu wa kunyonya wa mfalme Herode, na Sauli. Basi hawa walipokuwa wakimfanyia Bwana ibada na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia. Ndipo wakiisha kufunga na kuomba, wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao". (Matendo ya Mitume 13:1-3).*

Inaonekana baadhi ya watu walioorodheshwa katika kisa hiki ni sawa na wachungaji wa leo. Walikuwa wakimtumikia Bwana kwa pamoja katika kuomba na kufunga. Ingawa hatujaambiwa dhahirini masuala gani ambayo walikuwa wakiyaombea na kufunga, lakini bila shaka mioyo yao ilikuwa pamoja na Bwana, na ndiyo maana Bwana alizungumza nao. Bwana aliwataka viongozi hawa kutoka kanisa la Antiokia kumtengea Barnaba na Paulo kwa ajili ya kazi ambayo alikuwa amewaitia. Baada ya kutengwa huko kwa Barnaba na Paulo, yaliyoendelea ni historia (hayatuhusu). Antiokia lilikuwa ni kanisa lenye wachungaji wanaosikiliza, wachungaji na viongozi waliokuwa na mguso mkubwa katika ulimwengu hata kuzidi kanisa la Yerusalemu lenyewe.

Jambo la muhimu hapa ni hili: Wakati agizo kuu lilipotolewa na Kristo kuwaamuru wafuasi wake kuwa mashahidi wake kote hadi mwisho wa dunia, hakuna mtu ambaye angetabiri kwamba kanisa lililoanzishwa huko mbali kabisa katika nchi ya Syria lingekuwa na ushawishi wa kushangaza katika ulimwengu. Kama ungeniuliza mimi juu ya kitu gani kilileta tofauti, ningesema, ni "viongozi wanaosikiliza",

Ni kweli, wakati Petro akiwa bado huko Yerusalemu akitetea uwepo wake nyumbani mwa Kornelio, Mungu alikuwa tayari akiinua viongozi katika kanisa la Antiokia kupitia Roho wake. Viongozi hawa waliweza kusikiliza sauti yake wakati walipokuwa wanaendelea kumtumikia Mungu na kumwabudu. Walikuwa manabii na walimu, na walikuwa makini kwa Bwana. Mioyo yao ilikuwa ulipokuwepo moyo wa Bwana, na Bwana aliwakuta wakiwa tayari kubeba agizo lake.

Mungu aliwapa fursa ya kumtuma mmoja wa mitume wakuu waliowahi kutokea duniani. Na matokeo ya utume huo yalikuwa ni kuandikwa kwa takribani theluthi mbili ya vitabu vya Agano Jipya. Mtume Paulo, pamoja na washirika wake, alikuwa miongoni mwa watu waliokuwa na ushawishi mkubwa katika vitabu vya Agano Jipya vilivyokubaliwa.

Hiyo iliwezekanaje? Ilikuwaje kanisa ambalo lilianzishwa na wahamiaji walioteswa na wakawa wakimbizi kupokea sehemu ya heshima na umuhimu katika mpango wa kazi ya Mungu wa ukombozi katika ulimwengu? Walikuwa na viongozi au wachungaji waliokuwa wasikivu kwa Mungu. Walifunga, walihudumu na walisikiliza.

Wachungaji ni watu muhimu sana katika jambo ambalo Mungu anaweza kulifanya kwa kanisa lake. Si ajabu Paulo aliwaonya wazee wa Efeso kwa kuwaagiza kujitunza wao wenyewe na kulitunza kundi ambalo Roho Mtakatifu aliwaweka kuwa wasimamizi. Wachungaji hawa wangeweza kulikuza au kuliangamiza kundi. Wangeweza kuwatia moyo watu wa Mungu katika wito wao mkuu au kuwazuia wasiusikie wito huo. Wanachukua nafasi ya kushangaza katika maisha ya kanisa la Mungu na watu wake. Ni Makanisa mangapi kama ya Antiokia ambayo Mungu anayo huko ulimwenguni, yenye wachungaji watakaoweza kuisikiliza sauti yake?

Wito huu bado unaendelea hata leo, na wachungaji wasikivu bado wanausikia. Sababu ambazo Mungu alitaka atengewe Barnaba na Paulo bado ni zile zile hata leo. Paulo ameziandika kwa muhtasari katika Matendo 26:18, *"Uwafumbue macho yao, na kuwageuza waliache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi".*

Watu wengi bado wanaishi na kufa bila kuisikia habari njema za Mungu. Zipo jamii nyingi leo, majiji na miji ambayo bado haimjui Kristo kabisa, au sehemu ambazo Yesu aliwahi kujulikana hapo kabla lakini kwa sasa hajulikani tena. Mungu aliyeliita na kuliagiza kanisa laAntiokia bado anaita na kutuma leo: "Nitengeeni!" Je, wachungaji wanamsikia? Kama wewe ni Mchungaji, uko tayari kufanya nini kuhusiana na wito huu?

***Picha: Mch. Dk. Joshua Bogunjoko, Mkurugenzi wa SIM Kimataifa.***

# WACHUNGAJI NI UFUNGUO WA MAONO YA KANISA JUU YA UMISHENI


PICHA NA JONI BYKER

Mungu amewachagua wachungaji ili kulielekeza na kuliongoza kanisa lake. Ni maono na kielelezo cha Mchungaji ambacho kitalielekeza kanisa na ushiriki wake katika umisheni. Kama unaongoza kanisa unaweza kulisaidia kusanyiko kufahamu na kupokea jukumu lake kwa ajili ya umisheni wa ndani na nje ya nchi. Kila mmoja anapaswa kujua kwamba sisi sote tuna sehemu ya kufanya katika mpango wa Mungu wa umisheni.

Unaweza kumtia moyo kila mkristo kanisani kwako ili ashiriki katika umisheni kwa kwenda au kutuma (kupitia kuomba na kutoa).

Fikiria juu ya kuhubiri ujumbe wa kimishenari kwa watu wa Mungu kila upatapo nafasi. Kanisa lako linaweza kuwa na kamati au mpango wa umisheni, lakini usiunde kamati ya kufanya yale ambayo kanisa lote linapaswa kufanya! Huu ndiyo mwanzo mkuu! Bila kujali lilipo kanisa lako kwa sasa, mara zote huwa kuna hatua za kuchukua pale inapokuja katika kufanya umisheni wa kuvuka utamaduni mmoja kwenda mwingine. Unaweza kusaidia wakristo wako kufika mahali ambapo watu wanaweza kusema, “Sisi ni kanisa linalojali na kufanya umisheni” na si kwamba “sisi tuwe ni kanisa lenye mipango ya umisheni tu” bali kutumika katika kazi za umisheni isiwe ni kitu cha kujadiliwa na watu sita tu katika ofisi ya kanisa.

Itakuwa ni jambo jema kiasi gani kama suala hili litakuwa katika kinywa cha kila mtu katika kusanyiko lote la kanisa! Badala ya umisheni wa kiulimwengu kujielekeza kwenye juma moja tu kila mwaka katika kampeni au kufanya kongamano kubwa, kwa nini msifuatilie kupata taarifa na changamoto za umisheni kipindi chote cha mwaka?

Safari za umisheni siyo tu kwa ajili ya makundi ya vijana. Bali ni Safari za kulitembelea kundi la watu ambao wanaishi na kufa bila Kristo katika nchi yako au katika nchi nyingine za jirani ili kufungua macho ya watu na kupanua maono yao. Wape washirika wa kanisa lako nafasi ya kushiriki katika safari za umisheni – ni safari za kubadilisha maisha!

## Haya hapa ni baadhi ya mawazo na mapendekezo ya kukusaidia kuliwezesha kanisa lako:


- Fanya kongamano la umisheni kwa kuwaalika wamishenari ili kutia moyo na kuhamasisha.
- Panga na uandae harambee ili kuchangia mfuko wa umisheni ili kanisa liweze kutoa. Hamasisha utoaji: kila mmoja, kuanzia watoto, anaweza kujifunza kutoa mara kwa mara na kwa moyo. Na pia kumwomba Mungu kuinua watu ili kuwa wamishenari. Kanisa lako liwe linawategemeza wamishenari. Mmishenari atahisi kuungwa mkono na kupendwa.
- Hakikisha unalea mmishenari au unda kikundi kinachohusika na umisheni.
- Sisitiza kazi za umisheni katika ibada kanisani kwa kutoa nafasi ya kuelezea kazi za umisheni. Lionyeshe kanisa lako umuhimu wa kujihusisha katika umisheni.
- Hamasisha kupitia shuhuda na habari za wamishenari na pia sifia historia za maisha yao kwa watu wako. Inapowezekana, tumia vielelezo kama bendera, ramani, picha, uwasilishaji wa kutumia kompyuta na projekta na vijarida.
- Tengeneza ubao wa matangazo au ukurasa kwenye mitandao ya kijamii kwa ajili ya umisheni: bandika ukutani picha za wamishenari wanaosaidiwa na kanisa lako.
- Jifunzeni kitabu cha Matendo ya Mitume: kihubiri kitabu hiki na uandae somo kwa kina kutoka katika kitabu hiki. Lisaidie kanisa lako kujifunza jinsi kitabau hicho kinavyosema kuhusu umisheni.

Imechukuliwa kutoka *Let’s Go!* (Mafunzo ya Maingiliano ya Wamishenari) yaliyotolewa na SIM Kimataifa, katika toleo la Aprili 2015.

# JINSI KANISA LETU DOGO LILIVYOKUZA MOYO MKUU WA UMISHENI

NA MCH. MOSES PAYE





Kama wachungaji, kwa kiasi kikubwa, tunaweza kusaidia kuonyesha mwelekeo wa makanisa yetu. Sehemu kubwa ya jukumu letu ni kutumia ushawishi wa kiroho kwenye maisha na mwelekeo wa watu walioko chini ya uangalizi wetu. Na ndiyo maana tunaitwa viongozi.

Kanisa letu la Evangelical Christian Fellowship (ECF) yaani 'Ushirika wa Kiinjili wa Kikristo' lililoko nje ya Jiji la Monrovia, nchini Liberia, tarehe 26 Juni 2016 lilifanya sherehe ya kuiaga familia ya wamishenari ambayo ilikuwa inaenda kufanya kazi ya Mungu katika maeneo ya vijijini nchini Liberia. Tunamtuma ndugu Dexter Brown na familia yake kwenda kwenye mkoa wa Kusini Mashariki ili kuinjilisha na kupanda makanisa. Ndugu Dexter alieneza kazi ya uinjilisti hadi vijiji vilivyoko katika sehemu za Sinoe na maeneo mengine yaliyo ndani zaidi.

Huu ni wakati wa kusisimua sana kwa familia ya kanisa letu, na tunamsifu Bwana kwa upendeleo na uongozi wa Roho kutuongoza hata kufika nje ya mipaka na mazingira ya kanisa letu na kuwashirikisha wengine habari za Injili.

Kanisa la ECF limekuwa likiisaidia familia ya Brown katika kutafuta msaada wa kipesa. Lakini zaidi sana kuwatia moyo wakristo wetu ili waweze kukubali na kushiriki kikanilifu katika kazi za umisheni.

## Kuufanya Umisheni Uangaze na Kuonekana kwa Watu

Haya yamekuwa ni maombi yangu tangu kuanzishwa kwa kanisa kwamba umisheni ungekuwa ndio kusudio kuu la ECF. Katika mikutano yetu tumekuwa tunamwomba Bwana atusaidie ili tuwe watu wanaojali umisheni. Kila mwaka huwa tunautenga mwezi wa Tano kwa ajili ya umisheni. Umisheni ni kitovu cha mahubiri, mafundisho, nyimbo za kuabudu na maombi yetu. Tunasisitiza wajibu, kipaumbele, uzuri na thawabu kwa ajili ya kufanya umisheni, ambayo itawafanya watu wetu kutiwa moyo na kuchukua hatua za kushiriki katika kazi za umisheni. Huwa tunatoa matoleo maalum kila juma la mwezi wa Mei, ambayo kwa kawaida sadaka hiyo hupelekwa kwenye Bodi ya Umisheni ya kanisa la Kiinjili la Liberia (Evangelical Church of Liberia - ECOL), ili kusaidia kazi zake za kihuduma.

Mwaka 2009 nilianza mpango wa mwaka mmoja wa kufundisha Biblia ili kuwaandaa viongozi kwa ajili ya kutoa huduma ya umisheni. Karibu watu wote waliopata hayo mafunzo sasa wanatumika katika kanisa kwa uaminifu. Baada ya Dexter Brown kumaliza mafunzo 2010-2011, alitumika kama shemasi na mwalimu wa Shule ya Jumapili ya watu wazima.

Kwa miaka kadhaa hapo nyuma, mimi na mke wangu tuliongoza safari za kwenda kuhubiri vijijni. Kwa kawaida tuliwatia moyo washirika wa kanisa katika kuambatana nasi. Wengine waliungana nasi kwa ajili ya kuwashuhudia wanakijiji habari za Kristo. Waliporudi nyumbani, waliwaambia washirika wengine habari za kusisimua kuhusu kazi na mahitaji. Huduma hii ilisababisha kuanzishwa kwa makanisa matatu katika vijiji vitatu. Dexter mara nyingi aliambatana nasi safarini, na nilimwona akikuza hamasa kwa ajili ya roho za watu pale alipokuwa anawaambia habari za Yesu. Uamuzi wake wa kwenda kwenye uwanja wa umisheni haukuwa wa ghafla kama ajali; bali Bwana alikuwa amemwandaa.

## Sababu ya kusherehekea

Kanisa la ECF lililopo Monrovia, lilianzishwa mwaka 2001, wakati vita ilipokuwa inaendelea nchini Liberia. Leo lina waumini 165, na tuna watu wanne ambao ni wahanga wa ugonjwa wa Ebola, wakiwemo yatima wawili.

Familia nyingi za kanisa, ikiwamo na familia ya Brown, waliwekwa chini ya karantini wakati ugonjwa wa Ebola ulipozuka. Mwanzoni mwa 2015, wakati ECOL ilipopiga mbiu kwa Makanisa mengine kutuma wamishenari kwenye mkoa wa Kusini Mashariki, tulikuwa mara kwa mara tukimwomba Mungu ili aguse mtu wa kwenda.

Miezi mitatu baadaye Dexter aliniambia, "Mchungaji, nina uhakika kuwa Bwana anataka mimi niende." Dexter alisikia wito wa umisheni tangu alipomaliza mafunzo ya Biblia.

Yeye na familia yake wamekuwa wakiomba kwa ajili ya uongozi wa Mungu, kwa hiyo wito kutoka ECOL ulikuwa ni uthibitisho na jibu. Kama mchungaji wa ECF, namtukuza Mungu kwa kubadilisha kanisa letu kuwa mwili wa "waendaji" na "waunga mkono"! Inatupa furaha isiyo na kifani kuona waumini kusaidia huduma za umisheni. Ni jambo ambalo kila kanisa linapaswa kulifurahia na kulifanya.

***Picha na Warwick Walker***

# WAJIBU WA MCHUNGAJI KATIKA KUANZISHA KANISA LENYE MTAZAMO WA UMISHENI

NA PHILIP KOFI TUTU

*Kufanya kazi miongoni mwa watu ambao bado hawajafikiwa ni muhimu sana katika kukuza hamasa kwa ajili ya umisheni ndani ya mioyo ya wachungaji na viongozi wa kanisa. Mtu mmoja aliwahi kusema kwamba, hatutakuwa na mzigo kwa ajili ya watu waliopotea mpaka hapo tutakapopata uzoefu unaoitwa "utakatifu wa kutotosheka". Na hiyo hutokea pale tunapojiweka wenyewe katika mahali ambapo tutajihisi kuwa hatujatosheka- mahali ambapo mioyo yetu itavunjika na itanyenyekea kwa ajili ya waliopotea, mdogo na wa mwisho.*

Kuingia kwangu katika umisheni ilikuwa ni pale nilipoanza kutumika miongoni mwa watu wa Dangme, wanaoishi kusini mwa Ghana karibu na mto wa Volta. Niliingia kikamilifu kwenye huduma ya kichungaji mwaka 1981, na kanisa langu lilinituma kutumika kwa waDangme.

Ilikuwa ni huduma ngumu na yenye changamoto. Nilipoenda mara ya kwanza, nilikuwa peke yangu. Niliogopa kwenda pamoja na mke wangu kwenye eneo hilo. Dini ya Voodoo ambayo inaamini sana katika uchawi ilikuwa na nguvu sana katika eneo hilo. Ukiongea kinyume na miungu yao au ibada zao za sanamu, wangeweza kukushambulia. Lakini Mungu alikuwa mwema na alitulinda.

Tulipanda makanisa saba miongoni mwa waDangme na uzoefu huu uliumba hamasa ndani yangu kuwa na huduma ya umishenari. Miaka 10 baada ya kuondoka kwetu, ilikuwa vizuri kuona bado uwepo wa Mungu ulikuwa pale. Tulirudi makao makuu ya nchi yetu ambapo tulihusika na huduma kwenye maeneo ya mijini kwa miaka miwili. Uzoefu wangu wa mwanzo ulinifunza kuwa hakuna kanisa litakalokuwa na mafanikio mpaka litakapokuwa na maono ya umisheni, na kwa hiyo nilidhamiria kuona kila mchungaji anapata fursa ya kimisheni kila mwaka. Safari fupi fupi ni muhimu, na zinapaswa kuhusisha wazee wa kanisa pia. Wanaporudi huwa na mwanga mpya katika macho yao, ili kulihamasisha kanisa kuhusu umisheni na changamoto zake.

## Chukua hatua ya kuongoza!

Ni lazima tushirikishe maono kwa ajili ya kazi za Umisheni makanisani mwetu. Hata hivyo, kama unaamini katika kitu fulani lakini hukizungumzii kabisa kitu hicho, hapo kuna tatizo mahali fulani. Na hii yaweza kusababishwa na vikwazo vingi kuinuka vichwani mwao. Vikwazo hivi vinaweza kuwa ni pamoja na mazoea au mapokeo ya kiutamaduni (hivi sivyo tulivyozoea kufanya mambo yetu), mtazamo (hatuko tayari kufanya hili), msimamo wa kimadhehebu (hii siyo sera ya kanisa/dhehebu letu); na vizuizi vya kisiasa (hii inaweza kuwa hatari).

Wakati ambapo makanisa yanapoanza kujihusisha na umisheni, kila kitu hubadilika. Maisha yao ya maombi hubadilika na huanza kuwa na mtazamo mpana katika kumtumikia Mungu kuliko kuangalia mambo yao wenyewe. Wanaona mahitaji yanayowazunguka na mioyo yao huvunjika. Na huanza kuwa huru zaidi kuachilia watu na fedha kwa ajili ya kazi ya Mungu.



Kanisa la Afrika linayo nguvu ya ndani. Baadhi ya makanisa yetu yenye watu wengi hayakupokea misaada kutoka nje. Kwa hiyo, tunaweza kuwatia moyo na wengine; kanisa ambalo limekua kutokana na nguvu ya ndani linawezekana kila mahali.

Nchi za Magharibi zilituma wamishenari ili tuweze kuisikia Injili. Sasa ni zamu yetu kufanya yale yale kwa kutoka ili kuwafikia wale ambao bado hawajamjua Yesu. Afrika isingeweza kusikia habari njema isipokuwa kwa gharama iliyolipwa na wengine. Huu ni wakati wetu wakujitayarisha ili kuwa faraja kwa wengine na kuwa tayari kuhatarisha maisha yetu kwa ajili ya Injili. Tunamtumikia Mungu Mmishenari na Umisheni ndiyo mapigo ya moyo wa wake (Mwanzo 3; Isaya 6; Yohana 3:16). Kuwafikia wengine kwa Injili kutakugahrimu muda wako na fedha yako--- inaweza kuwa hata maisha yako. Itakugharimu kila kitu. Lakini wewe NENDA tu! Yesu alikuwa tayari kupata hasara ya vyote, kwa hiyo, tunapaswa kufuata mfano wake. Wachungaji, ninawatieni moyo katika kuongoza, kuelekeza na kuendeleza katika kujenga makanisa yenye afya bora ambayo yana shauku kubwa kwa ajili ya umisheni kote ulimwenguni.

*Mchungaji Philip Kofi Tutu, ni Mkurugenzi na Mwenyekiti wa Baraza la SIM huko Madina - Acra, Ghana, na pia ni mwalimu wa wachungaji juu ya uongozi, uinjilisti na umisheni. Philip na mkewe, Janet, wana watoto watano, ambao kwa sasa wana umri wa miaka kati ya 15 na 32.*

# NENDA! HABARI ZA KANISA LA AFRIKA LINALOHAMASISHA UMISHENI

## Mashua iliyo mbali

'Mashua iliyo mbali' ni filamu ambayo inalialika kanisa la Kiafrika katika kushikilia fursa ya kipekee ya kuwafikia Waafrika ambao bado hawajafikiwa na Injili; kwa kutoa changamoto kwa kanisa ya kuwa na nguvu kuu kwa ajili ya umisheni huko mbeleni.

Ni habari ya Max, kijana Mkenya anayeishi mijini. Max ana ndoto ya kupata kazi nzuri, rafiki na mchumba ambaye atamuoa baadaye. Baadaye Max anakutana na Yusuf, mvuvi na mwiislamu. Yusuf na watu wake hawana kanisa wala mkristo wa kuwashuhudia. Hali hii inamsukuma Max afikirie kama Mungu anamwita ili awe mmishenari.

Filamu hii ya dakika 120 ilitayarishwa na taasisi ya On Field Media (Huduma ya misheni ya AIM) kwa ushirikiano na washirika wengine. Inaonyesha gharama, vikwazo na namna ya kuvishinda kama kanisa linataka kuyafanya mataifa yote kuwa wanafunzi. Unaweza kuiangalia filamu hii kwenye https:// distantboat.com/swahil/.

## Mpango wa Umisheni wa Malawi unakuza Uinjilisti wa kuvuka mpaka

Makongamano ya kikanda ya wachungaji wenye wito wa kimisheni yaliandaliwa na SIM kwa ushirikiano na Chama cha Kiinjili cha Malawi. Makongamano hayo huchochea hamasa miongoni mwa makanisa ya Malawi kuvuka mpaka kwa ajili ya kuwafikia wengine. Matokeo yake yalikuwa ni kuanzishwa kwa mpango unaojulikana kama Mpango wa Umisheni nchini Malawi (Malawi Mission Intiative-MMI), ulioanzishwa mwaka 2013 na Ushirika wa Kiinjili wa Malawi (the Evangelical Association of Malawi-EAM) kwa ushirikiano na SIM.

MMI ni mtandao wa Makanisa yanayojali umisheni na wakala wa umisheni ili-kuwezesha uhamasishaji na kutoa msaada wa kazi ya umisheni wa kuvuka mipaka. Mchungaji Paul M.L. Mawaya wa SIM, ambaye ni mhamasishaji wa kitaifa nchini Malawi, anaendeleza kazi ya MMI kupitia Ukuzaji wa Ushirika wa Maombi wa Malawi. Vikundi hivi vya kuomba pamoja vinashiriki katika kupanga mafunzo, shughuli za uinjilisti, maombi na kuhamasisha makanisa kufanya umisheni kwa Waislamu. Pia husaidia wamishenari ambao wanahudumu katika maeneo ya umisheni na kuandaa makongamano ya kutia moyo watu kujitokeza na kuvuka mipaka ya kiutamaduni kwa ajili ya kazi za umisheni.

Mpaka sasa, Mchungaji Gusty na mkewe Ellina Makhutcha wametumwa kwenda kuhudumu kama wamishenari miongoni mwa kabila la Wayao ambao wanaishi nchini Msumbiji. Mchungaji Gusty anasaidiwa na Kanisa la Kibaptisti la Blantyre nchini Malawi. Katika ushirikiano huo huo Ndugu Francis Kuntenga ameanza kufanya kazi na kabila la Wayao huko nchini Malawi upande wa mpakani na Msumbiji.



### Tusaidie Tukusaidie

Je, una maswali kuhusu somo la toleo hili au mada zingine za kimisheni? Masomo gani ungependa AfriTWENDE iyashughulikie? Tunakaribisha mawazo yako ili kulifanya Gazeti letu kwenda na wakati na kubeba mada nyingi. Kwa maswali na maoni, tafadhali wasiliana nasi kwa barua pepe: afritwende@afrigo.org

**Kozi ya Kairos:** Kozi imeandaliwa ili kuelimisha na kutoa changamoto kwa wakristo na kulitia moyo kanisa kuitikia moyo wa Mungu kwa ajili ya umisheni kwa mataifa. Kairos inaelekeza na kuongoza huduma yenye mwamko na yenye maana katika kuvuka mipaka ya tamaduni na kuwa na nia ya kuwafikia wale ambao hawajafikiwa na habari njema za Yesu katika jamii zetu ili kumfanyia Mungu ibada.

Kairos inalenga maeneo manne ya umisheni ambayo ni: Msingi wa Kibiblia, Mtazamo wa Kihistoria; Mwelekeo wa Kimkakati; na hali ya Kiutamaduni. Inatumia zana za kuwawezesha kutimiza wajibu wao kikamilifu katika kufundisha, majadiliano, na mihadhara mifupi. Mafunzo ya Kairos yanaweza kukusaidia wewe na kanisa lako kufahamu kusudi la milele la Mungu juu ya umisheni toka kwenye kitabu cha Mwanzo mpaka Ufunuo wa Yohana. Wawezeshaji waliopata mafunzo na wenye hadhi ya kimataifa hufundisha kozi hii. Washiriki watasajiliwa na kupewa mbinu kwa ajili ya waliopotea.

Kwa Tanzania, kozi ya Kairos hutolewa kwa wiki moja kwa wachungaji, wainjilisti na wakristo waliojitoa wa madhehebu yote. Mafunzo haya hutolewa katika mikoa yote kwa lugha za Kiswahili and Kingereza. Kwa maelezo zaidi wasiliana na waratibu, Silas Brandl kwa barua pepe silas_brandl@gmx.de na Julius Rukya kwa simu namba +255754826533.



Picha: Jordi Zaragozà Anglès

# KWA NINI TUNAKWENDA MAKUNDI YA WATU: WADATOOGA

Wadatooga ni jina la ujumla kwa makundi ya Jamii moja ya wafugaji wnaohama yenye asili ya Nilotiki, ambao ni Wabarabaig, Wataturu, Rotigenga, Gidang'udiga, Simijiega, Burediga na Dalorajieaga. Watu hawa wanaishi zaidi sehemu ya kaskazini ya nyanda za juu za kivolkano zinazozunguka mlima Hanang' na Ngorongoro nchini Tanzania. Na kwa sasa wamesambaa sehemu nyingi za Tanzania mikoa ya Kati, Mashariki Pwani, Kusini na Magharibi Kusini mwa Tanzania. Wadatooga wanafuga mbuzi, kondoo, punda, lakini ng'ombe ndiyo mnyama muhimu na anayefugwa zaidi na jamii hizi. Jamii hizi zinaiishi kwa kuhamahama; na huenda popote kutokana na mahitaji ya mifugo. Kunatakiwa kuwe na mfumo wa watumishi kuhama na makundi ya Wadatooga wanapohamia vijiji vingine.

Wadatooga wanatazamwa na jamii zingine kama ni watu wagomvi na ndiyo maana wanachukuliwa kama maadui na hivyo kupewa majina kama wamang'ati (neno la Kimasai lenye maana ya adui). Watu hawa (Wadatooga) wanajipenda sana, pia wana sifa ya kuwa wapiganaji wakali. Wameshikilia tabia zao za asili na desturi zao, ikiwa ni pamoja na mtindo wao wa mavazi na lugha zao.

Wadatooga ni wagumu kuacha mila na kubadilika, ikiwa ni pamoja na kupokea imani ya Kikristo; wakishikilia kwa nguvu zote dini yao inayoamini juu ya Mizimu – mababu waliokufa siku nyingi. Wanaamini kuwa ukifa ukiwa mzee unakuwa huna dhambi na unaenda kuishi na Mungu na unaweza kuwasaidia wanaoishi kukabiliana na changamoto zozote za maisha. Ibada za Wadatooga hufanyika sehemu ambazo wanaamini ndiko sehemu Mizimu wanaishi, mfano makabulini, kwenye baadhi ya milima.

Kwa vile Wadatooga wengi hawazungumzi Kiswahili, ambayo ni lugha ya taifa la Tanzania na wengi wao hawajui kusoma na kuandika huwa ni ngumu kuwashirikisha injili, hivyo hulazimika kutumia lugha yao. Inakadiriwa kuwa ni asilimia 2 tu ndo wanamjua Yesu na asiilimia 98 hawamjui Yesu ni nani.

## Mahitaji ya Kuombea OMBA

1. Kwamba Injili iweze kupenya katika maeneo ya Wadatooga, kuongezeka na kuzaa matunda kwa ajili ya Wadatooga kupata uhuru wa kweli katika Kristo kutoka kwenye dini za asili na ibada za mababu.
2. Kwa ajili ya watumishi wanaohudumu katika maeneo haya ili waweze kutiwa nguvu na faraja.
3. Ili kwamba Mungu aongeze watenda kazi walio tayari kwenda na kuishi miongoni mwao na kuwashirikisha injili kwa jaili ya mioyo yao.
4. Kwa ajili ya waamini wapya waweze kuishika imani na waweze kuzifikia familia na jamii.
5. Kwamba Mungu alainishe nafsi zao na kubadilisha mitazamo yao ili waukubali ukristo na kuacha upinzani dhidi ya Injili.


SIM By Prayer — AFRICA INLAND MISSION

**AFRITWENDE**: afritwende@afrigo.org **AFRIGO**: info@afrigo.org **ALLONS-Y !** : info@afrigo.org **AFRÍDE** : afride@afrigo.org

**SIM East Africa**
Tel: +251 911 206 530
east-africa.office@sim.org

**SIM West Africa**
Tel: +233 30 222 5225
wamo.personnel@sim.org

**SIM Southern Africa**
Tel: +27 21 7153200
za.enquiries@sim.org

**AIM International**
amc.io@aimint.org
aimint.org/africanmobilization/